

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

01

KISWAHILI

Muda Saa 1:30

Mwaka: 2019

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **matano (5)**.
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A, B, C, D na E zina alama **kumi (10)** kila moja.

SEHEMU A (Alama 10)

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(iv) _____

(v) _____

SEHEMU B (Alama 10)

2. Badili majina yafuatayo kuwa vitendo. Kipengele cha cha (i) kimetumika kama mfano.
 - (i) Mchezo – cheza
 - (ii) Maombi –
 - (iii) Pigo –
 - (iv) Wimbo –
 - (v) Wazo –
 - (vi) Kilimo –

SEHEMU C (Alama 10)

3. (i) Kamilisha methali ifuatayo. “Jungu kuu _____”
- (ii) Anadika methali inayotumka kumuonya mtu anayependa kuchagua sana vitu hatimaye kupata kitu kibaya.
- (iii) Andika methali inayohimiza watu kufanya kazi kwa kushirikiana.
- (iv) Msema kweli mpenzi wa Mungu “Methali hii inatufundisha nini?”
- (v) Tegua kitendawili kisemacho “Bibi hatui mzigo wake”

SEHEMU D (Alama 10)

4. Kamilisha nafasi zilizo wazi kwenye barua kwa kuchagua majibu sahihi uliyopewa kwenye kisanduku.

Madhumuni,	S.L.P 100,	Zawadi,	2021,	13/11/2018
------------	------------	---------	-------	------------

Mpendwa Mama, shikamoo.

Ni Imani yangu kuwa mnaendelea vizuri na shughuli za kilimo. Naamini pia ndugu zangu wengine hawajambo hapo nyumbani.

(ii) _____ya barua hii ni kutaka kukujulisha kuwa, nimefauluUpimaji wa Kitaifa Darasa la Nne tuliofanya mwishoni mwa mwaka jana.

Nimefurahi sana kwa kuwa nimefaulu vixuri kwa kupata daraja A. Ni matumaini yangu hata mdogo wangu Furaha atafaulu Upimaji wake wa Darasa la Nne wa mwaka (iv) _____

Ninashukuru kwa kunihimiza kusoma kwa bidi, kufaulu kwangu kumetokana na maneno yako ya hamasa.

Kwa leo sina mengi Zaidi, ninaomba uwasalimie wadogo zangu wote.

Ni mimi mwanao (v) _____

SEHEMU E (Alama 10)

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Tusidharau wazazi, heshima kuwafanyia,
Wanafanya kubwa kazi, kutuzaa kutule,
Wanatupa na mavazi, sisi tunachekelea,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Wanatutunza vizuri, kwa chakula na mavazi,
Wananunua sukari, chai pia na maandazi,
Wanapika na achari, wanatupa na malazi,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Vilevile zahanati, tunakwenda kutibiwa,
Twaenda kila wakati, Ugonjwa tukizidiwa,
Hutupepea kwa dhat, kwa joto tukizidiwa,
Wazazi wetu ni nguzo, kwetu sisi wana wao.

Maswali:

- i. Shairi hili linahusu nini? _____
- ii. Neon “malazi” lina maana gani kama lilivyotumiak katika ubeti wa pili? _____
- iii. Je, mshairi anahitaji watoto wawafanyie nini wazazi wao? _____
- iv. Katika ubeti wa tatu, mshairi anasema watu wakiugua hupelekwa wapi? _____
- v. Shairi hili linatoa funzo gani? _____